


# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA RAIS



### TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI.



Tarehe 02/11/2021

#### MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 02/11/2021 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI.

##### A. WALIOHUDHURIA

1. Ndg Jeswold Ubisimbali	DLNRO	Mwenyekiti
2. Goleth Mdesa	Ag HPMU	Katibu
3. Ndg Elias Jamvia	DLFO	Mjumbe
4. Ndg Felix Tossi	Ag EO	Mjumbe
5. Mikidadi Nasoro	Ag DHRO	Mjumbe

##### B. WAALIKWA

1. Eng. Alex Foya	Mhandisi
2. Method Msokele	Mwanasheria

##### C. SEKRETARIET

1. Noel G. Nkana	Afisa ugavi
2. Mwangaza Kusenge	Afisa ugavi Mwandamizi
3. Grace Kombole	Afisa ugavi msaиди

#### BZ/01/04/2021/2022: KUFUNGUA KIKAO.

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao cha Bodi ya zabuni na kuwaomba kujadili agenda kwa makini na uwazi katika agenda zitakazoletwa kikaoni. Mwenyekiti alifungua kikao saa 6:10 mchana.

#### BZ/02/11/2021/2022: KUTHIBITISHA AGENDA

Agenda zilisomwa mbele ya Wajumbe wa Bodi ya zabuni, wajumbe wote walipokea na kuthibitisha agenda hizo ambazo ni: -

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha ajenda
3. Kusoma na kuthibitisha ajenda muhtasari wa Bodi ya zabuni wa tarehe 05/09/2021
4. Ombi la kibali cha utekelezaji wa miradi ya Covid 19 kwa njia ya Force Account
5. Mengineyo
6. Kufunga kikao

**BZ/03/11/2021/2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO  
CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 3/09/2021.**

Katibu kusoma Muhtasari wa kikao cha Bodi ya zabuni cha tarehe 22/03/2021. Wajumbe walipitia ukurasa kwa ukurasa na walifanya marekebisho kwa baadhi ya maneno katika muhtasari huo.

Wajumbe walipokea na kuthibitisha kuwa ni kumbukumbu sahihi ya vikao vya Bodi ya Zabuni.

**2. BZ/04/11/2021/2022: OMBI LA KIBALI CHA UTEKELEZAJI WA MIRADI  
YA COVID 19 KWA NJIA YA FORCE ACCOUNT**

Katibu wa bodi ya zabuni alitoa taarifa kwa bodi ya zabuni kuwa HImashauri imepokea jumla ya shilingi 2,150,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 99, bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalumu Pamoja na ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa Afya. Idara za Elimu Msingi, Sekondari na Afya ziliwasilisha maombi ya kibali cha ujenzi wa miundombinu ya **COVID 19** kuitia njia ya force akaunti.

**MAPENDEKEZO YA BODI YA WAZABUNI**

Wajumbe wa bodi ya wazabuni kwa pamoja waliridhia na kushauri kuwa utekelezaji huo kwa njia ya force akaunti utumike kwa kuzingatia taratibu, sheria na kanuni ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati.

**BZ/08/05/2021/2022: MENGINEYO.**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kama kuna mjumbe ye yeyote mwenye mengineyo.

Hakukua na mjumbe wa bodi ye yeyote mwenye mengineyo.

**BZ/14/05/2020/2021: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushiriki wao mzuri katika kikao hicho. Pia aliwaomba kudumisha umoja katika utendaji kazi ili kuleta maendeleo kwa wananchi wa Mufindi.

Mwenyekiti alifunga kikao mnano saa 8:35 mchana.

**UMETHIBITISHWA**

Saini .....

**Katibu**

Tarehe 04/11/2021

Saini .....

**Mwenyekiti**

Tarehe 04/11/2021